**UGANDA MARTYRS UNIVERSITY**

**DEPARTMENT OF KISWAHILI, 2024.**

**SEMISTER TWO**

**YEAR ONE**

**BACHELOR OF EDUCATION PRIMARY**

**KLE 61201: KISWAHILI GRAMMAR AND LEXICOLOGY**

**SEHEMU A**

**(Kiswahili Lexicology)**

1. (a). Fafanua maana ya dhana Leksikolojia na leksikografia (Alama 10)

(b). Fafanua mbinu za uundaji wa maneno (Alama 15)

2. Jadili changamoto zinazokumba wanaleksikografia katika shughuli ya uundaji wa kamusi.(Alama 25)

3.(a) Fafanua maana ya neno kamusi(Alama 05)

(b). Fafanua hatua zote za uundaji wa kamusi (Alama 20)

4. (a).Taja na ueleze aina za kamusi (Alama 17)

(b)Fafnua sababu za uundaji wa kamusi.(Alama 18)

**SEHEMU B**

**(Kiswahili Grammar)**

5. Tambua aina hizi za maneno kama yanavyojitokeza katika kila sentensi zifuatazo.

(Vivumishi, Nomino, vielezi, Viunganishi)

a) Mhadhiri wetu ni mzuri
b) Baba na wataenda kanisani
c) Mbuzi amekula chumvi
d) Kiongozi bora ni mzalendo
e) Kamba ndefu imekatikakatika sana.

(Alama 25)

6. (a)Andika sentensi hizi upya huku ukitoa kinyume cha maneno yaliyopigiwa msitari katika Kila sentensi.

i. Mwalimu alinunua gari jipya
ii. Benki ya centenary iko mbali na kituo cha polisi.
iii. Chumba cha wageni ni kichafu.
iv. Alipoona nyanya yake alicheka.
v. Msichana mwembamba ndiye alishindwa mbio.

(Alama 15)

(b). Geuza sentensi hizi ziwe Kwa wakati uliopota Hali timilifu.

i. Gari lilipita pale jana.
ii. Kasisi alihutubia watu kanisani.
iii. Mvua ilinyesha siku hiyo.
iv. Mti uliangukia gari lake.
v. Serikali ilipinduliwa na wanajeshi.

(Alama 10).

7. (a) Andika sentensi hizi kwa Hali ya kukubali

i. Asiyekujua hakuthamini
ii. Asiyejua neno haambiwi neno.
iii. Asiyesikia la mkuu hunvujika guu.
iv. Sijasikitishwa na udanganyifu huo.
v. Hatukukukumbuka tulipokuona.

(Alama 15).

(b). Andika sentensi hizi Kwa Hali ya kutendwa.

i. Paka aliua panya.
ii. Rais alitangaza kuongezeka kwa bei ya mafuta.
iii. Mwizi alivunja dirisha la nyumba.
iv. Mzee alikalia kigoda.
v. Kuku alitaga mayai thelathini.

(Alama 10)